

**MKATABA WA UNUNUZI WA VIFAA VYA UMEME NA VIYOYOZI KWA
AJILI YA UKARABATI WA MEDICAL CLINIC KUWA CHUMBA CHA
TIBA MTANDAO (TELEMEDICINE) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA
MKOA-IRINGA**

KATI YA

**MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA -
IRINGA**

NA

**MPULULU ENTERPRISES
IRINGA**

MKATABA WA UNUNUZI WA VIFAA VYA UMEME NA VIYOYOZI KWA AJILI YA UKARABATI WA MEDICAL CLINIC KUWA CHUMBA CHA TIBA MTANDAO (TELEMEDICINE) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA-IRINGA

MGANGA MFAWIDHI _Sanduku la Posta 260 Iringa ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mwajiri kwa upande mmoja.

MPULULU ENTERPRISES-IRINGA ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mzabuni kwa upande mwingine

KWA KUWA Mnunuzi anahitaji na yuko tayari kununua vifaa vya umeme na viyoyozi kwa ajili ya miundo mbinu ya mtandao vyenye thamani ya fedha shilingi **5,300,000/=** sawa na mchanganuo umeambatanishwa

HIVYO BASI pande zote mbili zinashuhudia makubaliano yafuatayo:

1. **KWAMBA** Mkataba huu ni wa mauziano ya **vifaa vya umeme na viyoyozi** Muuzaji atawajibika kuwasilisha vifaa hivyo ndani ya siku **tano** tangu kusainiwa kwa mkataba
- 2.
3. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kuuza **vifaa vya umeme na viyoyozi** kulingana na orodha ya vifaa vilivyoorodheshwa katika nukuu ya bei iliyoambatanishwa katika mkataba huu
4. **KWAMBA** Bei iliyonukuliwa katika fomu ya nukuu ya bei iliyoambatanishwa haitabadilika katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.
5. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kutoa vifaa kulingana na orodha ya vifaa vilivyo katika fomu ya nukuu ya bei
6. **KWAMBA** Malipo yatafanywa baada ya **vifaa vya umeme na viyoyozi** kupokelewa na kukaguliwa kama ni timilifu na vinakidhi ubora unaotakiwa
7. **KWAMBA** Mkataba huu utafika kikomo baada ya vifaa kupokelewa na taratibu za malipo kukamilika

8. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kufanya kazi kwa uaminifu na pasipo kumsababishia hasara yoyote mwajiri.
9. **KWAMBA** Mnunuzi atakuwa na wajibu wa kuvunja mkataba muda wowote atakapoona inafaa, pale atakapojiridhisha kuna ukiukwaji wa makubaliano katika mkataba
10. **KWAMBA** Endapo kutakuwa na hasara yoyote iliyosababishwa na muuzaji. Muuzaji atakuwa na wajibu wa kulipa gharama za hasara alizosababisha au kukatwa malipo yake ilikufidia hasara iliyosababishwa
11. **KWAMBA** Endapo kama kutakuwa na ucheleweshwaji wa kazi uliosababishwa na muuzaji, mnunuzi atakuwa na wajibu wa kuvunja Mkataba
12. **KWAMBA** Mnunuzi atatoa kusudio la kuvunja Mkataba kwa maandishi ndani ya siku tatu
13. **KWAMBA** Mkataba huu ni halali kwa mujibu wa sheria za Tanzania na utatafsiriwa kwa mujibu wa sheria hizi.
14. **HIVYO BASI** Pande zote mbili zimeweka saini tarehe , mwezi na mwaka kama inavyoonyesha hapa chini:

Kwa ajili ya ushahidi wa makubaliano ya utekelezaji wa mkataba huu, pande mbili zinazohusika wameweka saini zao kama ifuatavyo:

YAMESAINIWA NA KUTOLEWA NA

Saini:.....

Jina:..... *Alfred Laiso* -

Cheo: MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA-IRINGA (MNUNUZI)

Tarehe:..... *22.6.22*

Saini :..... *[Signature]*

Jina: *Ho Bokela* *Kamatula*

Cheo: **SHAHIDI UPANDE WA MNUNUZI**

Tarehe..... 22/06/2022

YAMESAINIWA NA KUTOLEWA NA

Saini: David.....

Jina: DAVID MPULULU.....

Cheo: **MUUZAJI**

Tarehe;..... 22/06/2022



Saini: Jason.....

Jina: Henrieth Jason.....

Cheo: **SHAHIDI UPANDE WA MUUZAJI**

Tarehe:..... 22/06/2022